**Bwana Yesu Asifiwe...**

Kwanza, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupatia fursa hii ya kipekee kushiriki kilele cha maadhimisho ya miaka 50 ya *New Life Outreach*. Mimi binafsi ninayo furaha kubwa kujumuika nanyi na kupokea baraka inayotokana na kazi ya kichungaji ya *New Life Outreach*. Aidha, naushukuru uongozi wa *New Life Outreach* kwa kumwalika Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa Mgeni Rasmi katika Maadhimisho haya. Mheshimiwa Rais alipenda kushiriki nanyi siku ya leo, lakini haikuwezekana kutokana na majukumu mengine aliyonayo nje ya nchi. Hivyo, amenituma mimi kumwakilisha na kuwasilisha kwenu salamu zake nyingi za upendo na pongezi za dhati kwa adhimisho hili kubwa la Jubilei ya miaka 50 ya huduma ya *New Life Outreach*.

Nami naungana na Mheshimiwa Rais kumshukuru Mungu kwa matunda mengi yatokanayo na mbegu iliyopandwa na Dkt. Egon Falk na Mama Hannah, miaka 50 iliyopita. Aidha, Serikali inaungana na Waumini wote wa New Life City Church kumshukuru Mungu kwa kazi njema, tena yenye mafanikio makubwa, ambayo ni pamoja na kutangaza Injili kupitia mikutano, semina, warsha na makongamano, kuanzisha Chuo cha Biblia, shule za sekondari, msingi na awali na vile vile kuandaa watumishi wengi wa kiroho ambao wanaendeleza huduma katika maeneo mbalimbali, ndani na nje ya nchi yetu. **Hongereni sana**.

**Waheshimiwa Viongozi wa Kanisa na Wananchi wenzangu;**

Pili, napenda kuwasilisha shukrani za dhati za Serikali kwa *New Life Outreach*, kwa huduma bora na zisizo na ubaguzi mnazotoa kwa jamii ya Watanzania, hususan katika sekta za elimu na malezi kwa vijana. Ninafurahi kusikia kwamba baadhi ya vijana ambao *New Life Outreach* imewafadhili kimasomo, wamefanikiwa kuhitimu katika ngazi mbalimbali za elimu na kuanza kuishi maisha ya kujitegemea. Serikali inatambua na kuthamini jitihada za madhehebu ya Dini ya kumwinua na kumstawisha mwanadamu kiroho na kimwili. Hivyo, ninawahakikishia kwamba Serikali itaendelea kuenzi mchango mkubwa wa madhehebu ya Dini, katika utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii. Kwa niaba ya Serikali napenda kuwahakikishia kuwa itaendelea kusimamia na kulinda haki ya kuabudu kwa wananchi wote kwa mujibu wa ibara ya 19 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kwamba wananchi wanaendelea kuishi katika mazingira ya haki na amani.

**Waheshimiwa Viongozi wa Kanisa na Wananchi wenzangu;**

Pamoja na kuwa leo ni siku ya furaha na shukrani kwa Mungu kwa kazi kubwa iliyofanywa na inayoendelea kufanywa na New Life Outreach hapa nchini, napenda kutumia hadhara hii kuzungumza na Watanzania kuhusu changamoto tatu kubwa zinazolikabili Taifa, ambazo ninaomba ushirikiano zaidi kutoka kwa viongozi wa dini, ili kwa pamoja tuzipatie ufumbuzi na kuepuka madhara zaidi.

**Kwanza**, hivi sasa yameibuka mafundisho ya baadhi ya viongozi wa dini yanayowaaminisha wafuasi wao kutegemea miujiza zaidi ili kupata maendeleo badala ya kufanya kazi kwa bidii. Viongozi hao wanawaelekeza waamini wao kwenda kwenye nyumba zao za ibada wakaombewe ili wapate mali (magari, nyumba, pesa) wanazozitamani au kutatuliwa shida zao. Tunashuhudia kuongezeka kwa wahubiri wanaojilimbikizia fedha na mali binafsi kutokana na sadaka na mauzo ya vitu mbalimbali kama maji, mafuta na udongo. Wengi wa wahanga wa mahubiri ya aina hiyo ni wananchi wanyonge wanaokabiliwa na shida au matatizo mbalimbali ya maisha yakiwemo magonjwa, umaskini, migogoro katika ndoa, ugumba, kukosa ajira n.k. Vilevile, inasikitisha sana kuona kwamba wapo pia wahubiri wachache wanaoshabikia wazi wazi maovu, kama ndoa za jinsia moja, ushoga, ulawiti n.k., matendo ambayo ni chukizo mbele ya Mungu. Lakini, kama tunavyofahamu, dini ya kweli ndiyo dhamiri (conscience) ya jamii inayopaswa kutuongoza vema kuutambua na kuuishi ukweli unaotoka kwa Mungu. Tunasoma katika Yakobo 1: 27 kuwa "Dini ya kweli ni kujitoa kwa Mungu na kuwasaidia yatima na wajane katika shida zao na kujilinda mwenyewe usichafuliwe na mambo ya ulimwengu" *(True religion is a devotion to God, demonstrated by love and compassion for fellow men, coupled with unworldliness)*. Kwa sababu hiyo, kupitia maadhimisho haya, ninawaomba sana viongozi wetu wa dini, tena kwa unyenyekevu, waungane na Serikali kukemea vikali mafundisho na matendo hayo yasiyofaa katika jamii yetu na yasiyozingatia sheria za nchi yetu. Aidha, nasi viongozi wote tuwahimize wananchi kufanya kazi kwa bidii, maarifa na uzalendo, huku wakimuomba Mwenyezi Mungu abariki kazi zao. Na sisi viongozi tuwe wa mfano katika hili.

Ninawakumbusha pia viongozi wa Wizara ya Mambo ya Ndani, kupitia Ofisi ya Msajili wa Jumuiya, kusimamia kikamilifu Sheria ya Usajili wa Jumuiya (The Societies Act, Cap 337, pamoja na Kanuni zake za 2001 na Sheria Na. 03 ya 2019) ili kuhakikisha kuwa Taasisi (ambazo zinajumuisha Taasisi za kidini) zinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia malengo na masharti ya usajili wake.

**Waheshimiwa Viongozi wa Kanisa na Wananchi wenzangu;**

**Changamoto ya pili,** inahusu mmomonyoko wa maadili katika jamii yetu. Hivi sasa, kuna kasi kubwa ya mmomonyoko wa maadili katika jamii. Mmomonyoko huu unaonekana miongoni mwetu wazazi/walezi na hata kwa vijana na watoto wetu. Kutokana na matumizi holela ya mitandao ya kijamii, jamii yetu na hususan vijana wengi, wanadhani kwamba ili kuwa kijana wa kisasa, inawalazimu kuiga mambo yanayooneshwa kwenye mitandao hiyo yakiwemo yale yasiyo endana na mila na desturi zetu. Hali kadhailka, tabia ya kutopenda kufanya kazi inazidi kuota mizizi katika jamii, ambapo baadhi ya vijana hawataki kufanya kazi katika sekta za uzalishaji mali kama kilimo na ufugaji ili kujipatia kipato na kujikimu kimaisha. Badala yake, wanatumia muda mwingi kwenye kamari au kucheza pool. Vijana hao wamegeuka kuwa tegemezi na baadhi yao hujihusisha na vitendo viovu kama vile wizi na unyang'anyi, matumizi ya bangi, shisha na dawa za kulevya, ulevi wa pombe, uasherati, ubakaji, ulawiti na ushoga. Vilevile, tunashuhudia kuongezeka kwa matukio ya mauaji ya kikatili, ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto na wanawake, familia za mzazi mmoja, watoto waliozaliwa nje ya ndoa, migogoro ya ndoa, talaka, migogoro ya mirathi na ardhi, ubadhirifu wa mali za umma na matukio ya watu kujinyonga.

Vile vile, ulevi, uzembe na kutozingatia sheria za usalama barabarani vimepelekea kushamiri kwa ajali mbaya za barabarani zinazogharimu maisha ya wananchi wengi mno. Mathalan, takwimu zinaonesha katika mwaka 2023 kulikuwepo matukio ya ajali za barabarani 1,733, ambapo vifo vilivyotokana na ajali hizo vilikuwa 1,647. Aidha, majeruhi wa ajali za barabarani walikuwa 2,716. Katika wiki hii peke yake, tena katika Mkoa mmoja tu wa Mbeya, nchi yetu imepoteza jumla ya watu 21 na wengine wasiopungua 40 kujeruhiwa. Vifo hivyo vinajumuisha watoto wadogo 4 chini ya umri wa miaka 8. Kwa upande mwingine, katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2023 kulikuwa na jumla ya matukio 435 ya ajali zinazohusisha pikipiki yaliyoripotiwa. Katika kipindi hicho hicho, idadi ya vifo vilivyotokana na ajali za barabarani zinazohusisha pikipiki ilikuwa 376. Mimi naamini kwa dhati kabisa, kwamba kiini cha maovu yote haya ni kukosekana kwa hofu ya Mungu miongoni mwa jamii yetu.

Napenda kutumia nafasi hii, kwanza kuwakumbusha madereva wote wa vyombo vya moto nchini kuzingatia sheria za usalama barabarani na kutambua kwamba wanabeba roho za watu na za kwao wenyewe. Aidha, ninawakumbusha wakaguzi wa magari wa LATRA na Kikosi cha Polisi cha Usalama Barabarani kukagua magari ili kudhibiti magari mabovu yasiingie barabarani na kuhakikisha vidhibiti mwendo vinafanya kazi, pamoja na kukagua sifa za madereva hasa wa Mabasi na Malori. Wamiliki wa Mabasi na Malori wahakikishe magari yao yanakuwa na madereva walau 2 kwa safari zote ndefu zinazozidi kilomita 300. Vilevile, TANROADS wahakikishe alama za tahadhari zinawekwa katika maeneo yote hatarishi ya barabara kuu. Pia, wasafiri wazingatie kufunga mikanda wakati wote wa safari na kutoa taarifa kwa Kikosi cha Usalama Barabarani pale dereva wa chombo wanachosafiria anapoendesha kwa mwendo mkali kupita kiasi. Na mwisho, ninawasihi viongozi wote wa dini kuzidi kuombea usalama wa wasafiri na vyombo wanavyotumia na kuwakumbusha waamini kuzingatia sheria za usalama barabarani.

**Changamoto ya tatu,** ni uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Uhai wetu katika dunia hii unatishiwa na uharibifu wa mazingira ambao umekithiri. Jitihada mbalimbali za kitaifa na kimataifa zimechukuliwa kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi lakini bado matokeo yake si ya kuridhisha hata kidogo. Uharibifu wa misitu na ukataji wa miti unaonekana katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, ikiwemo hapa mkoani Arusha. Aidha, uharibifu wa mazingira unadhihirika katika kukauka kwa vyanzo vya maji, maporomoko ya ardhi, kuziba kwa mifereji pamoja na barabara na madaraja kusombwa na mafuriko, utupaji hovyo wa taka ngumu ikiwemo plastiki, uchafuzi wa fukwe za Bahari na Maziwa na kuongezeka kwa magonjwa. Ninawasihi nyote kutambua kuwa Serikali pekee haitafanikiwa kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi endapo sisi wananchi hatutabadili tabia na kuchukua hatua za makusudi kulinda na kuhifadhi mazingira yetu. Nawaomba viongozi wa huduma ya *New Life Outreach*, viongozi wa dini wa madhehebu mengine na waamini wa dini zote kuzingatia mafundisho ya imani zetu yahusuyo wajibu wetu wa kuitunza vema dunia tuliyokabidhiwa na Mwenyezi Mungu, kama tunavyosoma katika Kitabu cha Mwanzo kuwa ***"Bwana Mungu akamtwaa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza"*** *(Mwanzo 2:15)*.

**Waheshimiwa Viongozi wa Kanisa na Wananchi wenzangu;**
Katika risala iliyosomwa hapa hivi punde nimesikia kuhusu changamoto ya ubovu wa barabara inayokwenda kwenye shule za *New Life Schools* pamoja na shule za Serikali za Kiranyi Sekondari na Shule ya Msingi Nyerere. Ninaitaka OR-TAMISEMI kupitia Wakala wa Barabara Vijijini (TARURA) kuifanyia matengenezo ili kuwaondolea adha wananchi na wanafunzi wanaotumia barabara hii.

Kabla sijahitimisha, napenda kuwakumbusha kuwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unatarajiwa kufanyika tarehe 27 Novemba mwaka huu. Ili kushiriki kwenye uchaguzi huu ni lazima taarifa za kila Mkazi ziingizwe kwenye Daftari la Kudumu la wapiga kura. Hivyo, ninawahimiza wananchi wote kujitokeza kuandikishwa wakati wa zoezi la kuboresha daftari hilo litakapofanyika hapa mkoani kwetu.

Napenda kuhitimisha salamu za Serikali kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kusisitiza kuhusu umuhimu wa kulinda na kudumisha amani tuliyonayo, Umoja wetu na Uhuru wa nchi yetu wakati wote. Mwisho kabisa, kwa mara nyingine tena nawapongeza sana Mwinjilisti Dkt. Egon Falk na Mama Hannah Falk kwa kazi kubwa na nzuri sana mliyoifanya kwa miaka hii 50. Ninawatakia baraka, afya njema na mafanikio katika utumishi wenu! Aidha, nawapongeza viongozi wote wa *New Life Outreach* Tanzania kwa kuendeleza kazi nzuri iliyoanzishwa na waasisi wa huduma hii na kuwezesha kupatikana kwa mafanikio makubwa katika kipindi hiki cha nusu karne. **Mwenyezi Mungu awabariki sana.**

**Bwana Yesu Asifiwe...!**
**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**